



## TAARIFA

### **WITO WA USHIRIKI WA TUZO YA KIMATAIFA UNESCO – AL FOZAN YA KUKUZA WANASAYANSI WACHANGA KATIKA SAYANSI, TEKNOLOJIA, UHANDISI NA HISABATI**

Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar kimepokea barua yenyewe Kumb. Na. AB.347/373/01A kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inayohusu wito wa maombi ya toleo la kwanza la Tuzo ya Kimataifa ya UNESCO –Al Fozan inayolenga kukuza wanasayansi wachanga katika Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati.

Taarifa Zaidi kuhusiana ushiriki ikiwemo sifa zinapatikana *online* kupitia *link* <https://unescoalfozanprize.org/>. Maombi yamefunguliwa rasmi kuanzia tarehe 1Juni, 2022 na mwisho wa kuwasilishwa ni kabla ya tarehe 15 Novemba, 2022.

Aidha unaweza kuuliza maswali kwa Sekreteriet wa Tuzo hiyo kupitia barua pepe [unescoalfozanprize@unesco.org](mailto:unescoalfozanprize@unesco.org).

Kwa hivyo, Uongozi wa Chuo unawashajiisha wanataluma kushiriki na kuwashajiisha wanafunzi wetu kwenye fani husika kushiriki kwa wingi. Wakuu wa Skuli mnaombwa kusimamia hili kwani mara nyingi fursa hizi zikija wafanyakazi na wanafunzi walio chini yetu hawashiriki ukilinganisha na vyuo vingine.

Ahsanteni.

**Imetolewa na Ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo- Taaluma  
Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar (SUZA).**